



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

KUKAMILIKA KWA ZOEZI LA UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA KATIKA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi, inatangaza kukamilika rasmikwa zoezi la Uandikishaji wa Wapiga Kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa mkoa wa Dar es salaam tarehe 04/08/2015 na hivyo kuhitimisha rasmi Uandikishaji wa Wapiga Kura kwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa *Biometric Voters Registration(BVR)* kwa nchi nzima.

Uandikishaji wa Wapiga Kura kwa Mkoa wa Dar es salaam ulianza rasmi Julai 22 na kufanyika kwa siku kumi (10) muda ambao haukutosheleza kutokana na idadi kubwa ya wananchi waliojitokeza hali ambayo Tume ililazimika kuongeza siku nne (4) zaidi. Hii inatafsiriwa kuwa imetokana na mwamko mkubwa wa wananchi waliojitokeza kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ikilinganishwa na miaka mingine iliyopita.

Hadi tarehe 04 Agosti, 2015 Mkoa wa Dar es Salaam jumla ya Wananchi waliojitokeza na kuandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ilikuwa kama ifuatavyo: Wilaya ya Kinondoni lengo lilikuwa 1,102,565 jumla ya Wapiga Kura waliojiandikisha ni 1,157,617 sawa na 105%, Wilaya ya Temeke lengo lilikuwa 896,142 imeandikisha jumla ya Wapiga Kura 886,564 sawa na 98.9%. Wilaya ya Ilala lengo lilikuwa

811,716imeandikisha Wapiga Kura 886,564 sawa na 98.9%, Kwa ujumla lengo la Uandikishaji Wapiga Kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa Mkoa wa Dar es Salaam lilikuwa 2,810,423 ambapo zoezi limeweza kuandikisha jumla ya Wapiga Kura 2,845,256 sawa na 101.2%.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kusesitiza kuwa hakutakuwa tena na muda wa nyongeza wa kuandikisha Wapiga Kura na kwamba zoezi linaloendelea hivi sasa ni la kuweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura pamoja na kutoa Fomu za kugombea Urais waliopitishwa na Vyama vyao vya Siasa. Tume inasisitiza kuwa hakutakuwa na muda zaidi wa Uandikishaji kwa kuwa Wagombea wa Vyama wanaochukua Fomu hivi sasa wanahitaji kudhaminiwa na wanachama ambao tayari wameisha jibandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Tume inaendelea na zoezi la Uwekaji Wazi (Display) wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambapo hadi sasa tayari mikoa kumi na tisa (19) imekwisha pelekewa Daftari la Awali la Wapiga Kura. Mikoa mingine ikiwemo Zanzibar na Dar es salaam mchakato wa kuandaa Daftari la Awali unaendelea na unatarajiwa kukamilika muda si mrefu kuanzia sasa baada ya Uandikishaji kukamilika. Uwekaji Wazi wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa mikoa iliyokwisha kupokea Daftari utanza 7 Julai, 2015 na utadumu kwa siku tano (5). Zoezi la Kuweka Wazi Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linafanyika ili kutoa fursa kwa wale wote waliojiandikisha kuweza kusahihisha taarifa zao, kuhamisha taarifa za Wapiga Kura waliohama toka Kata au Jimbo moja kwenda Kata au Jimbo jingine, kutoa kadi kwa Wapiga Kura waliopoteza kadi zao, kuangalia iwapo taarifa za

mpiga Kura aliyejiandikisha zipo kwenye Daftari na kuweka Pingamizi kwa jina au taarifa za Mpiga Kura asiye na sifa ya kuwemo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Sambamba na maandalizi ya Daftari la Awali, Tume inaendelea na zoezi la utoaji wa Fomu za Urasi kwa Wagombea Urais na Wenza wao ambapo hadi kufikia leo jumla ya Vyama vya Siasa vitano (5) tayari Wagombea wao wamechukua Fomu. Vyama hivyo ni United People Democratic Party (UPDP), Tanzania Labour Party (TLP), Democratic Party (DP), Chama cha Umma (CHAUMA) na Chama cha Mapinduzi (CCM). Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa wito kwa Vyama vingine kuharakisha mchakato wa kuwapata Wagombea wao na kuwasilisha Ratiba kwenye Makao Makuu ya Tume ili kuwezesha Tume kuendelea na hatua nyingine zinazofuata.

Kwa ujumla zoezi la Uandikishaji Wapiga Kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa Mkoa wa Dar es salaam na nchi nzima kwa ujumla limefanyika na kukamilika kwa mafanikio makubwa licha ya changamoto za hapa na pale zilizojitokeza hasa katika hatua za mwanzo za Uandikishaji. Tume inapenda kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika kufanikisha zoezi hilo.

Imetolewa na,

Mhe. Jaji Mst. Damian Z. Lubuva
MWENYEKITI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

